Al-Islam.org
Ahlul Bayt Digital Islamic Library Project
Published on *Al-Islam.org* (https://www.al-islam.org)

Hakika Tawassul uhalisi wake umeelezwa na Qura'ni tukufu pindi Mwenyezi Mungu alipowaambia waumini:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ وَابْتَغُوا إِلَيْهِ الْوَسِيلَةَ وَجَاهِدُوا فِي سَبِيلِهِ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ {35}

"Enyi mlioamini mcheni Mwenyezi Mungu na tafuteni njia ya kum- fikia. Na piganeni kwa ajili ya dini yake ili mpate kufaulu." Al-Maida: 35.

Hakika Aya hii tukufu imehesabu Uchamungu na Jihadi kuwa ni miongo- ni mwa njia za kisheria ambazo mwanadamu anaweza kuzifanya sababu ya kumfikia Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Na je, kuna njia nyingine ambazo zimehimizwa na Sheria? Au jambo hili ameachiwa mwanadamu na kwa uwezo wake agundue njia nyingine za kumkurubisha kwa Mwenyezi Mungu?

Ni wazi kuwa njia ambazo mja anaweza kujikurubisha kwazo kwa Mwenyezi Mungu hazitokani na Juhudi za kielimu, kwani kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu na njia za kupatikana ukuruba huo zinahitaji mwongozo wa Mwenyezi Mungu.

Na hapo ndipo Sheria ilipochukua jukumu la kuzibainisha, ikazitolea maelezo na kuziwekea mipaka ndani ya Kitabu na Sunna tukufu. Kila njia isiyokuwa ile iliyoelezwa na Sheria kwa namna ya pekee au ya mjumuisho, basi yenyewe ni aina moja ya bidaa na upotovu.

Imam Ali bin Abu Twalib amegusia njia ambazo kwazo mja atajikurubisha kwa Mwenyezi Mungu, akasema: **"Hakika njia bora ya kupita wenye kwenda kwa Mwenyezi Mungu ni: Kumwamini Yeye na Mtume wake na** Jihadi katika njia yake, hakika yenyewe ndio heshima ya Uislamu.

Na Tamko la dhati, hakika lenyewe ndio silika. Na kusimamisha Swala, haki- ka yenyewe ndio dini. Na kutoa Zaka, hakika yenyewe ni faradhi.

Na Funga ya Ramadhani, hakika yenyewe ni ngome dhidi ya adhabu. Na Kuhiji Nyumba tukufu na kufanyia Umra, hakika hivyo viwili vinaondoa ufakiri na kuondoa dhambi. Na kuunga undugu wa damu,

hakika kwenyewe ni ongezeko la utajiri katika mali.

Na Sadaka ya wazi, hakika yenyewe inaepusha kifo kibaya. Na kutenda wema, hakika wenyewe unazuia kushindwa kwa udhalili.”1

Qur’an tukufu imeelekeza mwenendo wa kusifika unaohitajika kwa waislamu, Mwenyezi Mungu akasema:

وَلَوْ أَنَّهُمْ إِذْ ظَلَمُوا أَنْفُسَهُمْ جَاءُوكَ فَاسْتَغْفَرُوا اللَّهَ وَاسْتَغْفَرَ لَهُمُ الرَّسُولُ لَوَجَدُوا اللَّهَ تَوَّابًا رَحِيمًا {64}

“Na lau wangelikujia walipojidhulumu nafsi zao wakaomba msamaha kwa Mwenyezi Mungu na Mtume akawaombea msamaha, bila shaka wangemkuta Mwenyezi Mungu Mwenye kupokea toba, Mwenye kure- hemu.” An-Nisai: 64.

Kwa waislamu utaratibu huu uliosifiwa haukomei kipindi cha uhai wa Mtukufu Mtume tu, hilo ni baada ya Mwenyezi Mungu kusema:

وَلَا تَحْسَبَنَّ الَّذِينَ قُتِلُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ أَمْوَاتًا ۚ بَلْ أَحْيَاءٌ عِنْدَ رَبِّهِمْ يُرْزَقُونَ {169}

“Wala usidhani wale waliouliwa katika njia ya Mwenyezi Mungu kuwa ni wafu, bali wako hai wanaruzukiwa kwa Mola wao Mlezi.”Al-Imrani: 169.

Hivyo yenyewe ni Ibada endelevu inayofanywa hata baada ya kifo cha Mtukufu Mtume, na waislamu waliifahamu ruhusa hiyo na wakaitenda baada ya kifo chake kama walivyosema baadhi ya wafasiri.2

Hivyo hakuna kizuizi cha mahusiano na Mwenyezi Mungu na kuomba msamaha kutoka kwake au kuomba kupata haja za kiakhera na kidunia kwa njia ya kupitia njia ya Mtukufu Mtume ili awaombee kwa kuzingatia ukuruba wake kwa Mwenyezi Mungu na nafasi yake maalumu kwake. Njia hii imehimizwa na Sheria na kuainishwa na Qur’ani tukufu. Kwa ufafanuzi zaidi tutafuatilia utafiti katika nukta zifuatazo:

Kwanza: Maana ya Tawassuli kilugha na kiistilahi.

Pili: Rai mbalimbali kuhusu hukumu ya Tawassuli.

Tatu: Ruhusa ya Tawassuli ndani ya Qur’ani.

Nne: Tawassuli ndani ya Hadithi za Mtume.

Tano: Mwenendo wa Waislamu katika Tawassuli. Sita: Tawassuli kwa mujibu wa Ahlul-Baiti.

Saba: Mjadala dhidi ya wanaokanusha ruhusa ya kisheria juu ya Tawassuli

1. Nahjul-Balagha, uhakiki wa Subhiyu Asw-Saleh: Hotuba ya 110/ 163.
2. Tafsiri Ibnu Kathir 1:532.

Source URL: https://www.al-islam.org/fr/tawasali-sayyid-abdul-rahim-al-musawi/utangulizi